

TAARIFA KUTOKA MANISPAA YA ØVRE EIKER KUHUSU CHANJO DHIDI YA COVID-19

Pata/chukua chanjo – jilinde wewe mwenyewe na wengine!

Lengo kuu la chanjo ya corona ni kulinda maisha na afya ya wale walio katika hatari kubwa ya kuugua na kushambuliwa vibaya na ugonjwa wa Covid-19. Chanjo hii kwa Norway ni ya hiari, na chanjo mpya dhidi ya Covid-19 ni bure.

Tunapendekeza uchukue chanjo mara tu/pindi unapopewa ofa ya chanjo hiyo.

Madhumuni ya chanjo ni:

- kupunguza hatari ya kifo
- kupunguza hatari ya ugonjwa mbaya na hatari
- kudumisha huduma muhimu na miundombinu muhimu
- kulinda ajira
- kuifungua tena jamii

Manispaa inawahimiza wakazi wote wenye umri wa zaidi ya miaka 18 kujiandikisha haraka iwezekanavyo katika ufumbuzi/suluhisho letu la kidijitali kwa chanjo, bila kujali kama unataka chanjo au la.

Jinsi ya kujiandikisha/kujisajili :

1) Jisajili/jiandikishe mwenyewe

2) Pata msaada kwa jamaa au mtu wa karibu

3) Piga simu ya chanjo

Chaguo1:

[Bonyeza hapa kwenda kwenye usajili](#). Bofya/bonyeza kwenye

kona juu upande wa kulia ikiwa unataka kubadiri lugha nyingine isipokuwa ya Kinorwei. Lazima uingie **na** BankID. Fuata maelekezo zaidi. Ikiwa **unataka** ofa ya chanjo, **tutatumia nambari ya simu iliyosajiliwa kukupa maelezo kuhusu ni lini itakuwa zamu yako ya chanjo.**

Chaguo2: Pata msaada kutoka kwa ndugu au jamaa wa karibu ili kujiandikisha.

Angalia chaguo 1, au [bofya hapa kwa maelezo zaidi](#) **(Kinorwei)**. Yeyote atakayekusaidia lazima aingie na BankID yake, na kisha aingize taarifa muhimu/husika kukuhusu. Tunatumia namba za simu ambazo zimesajiliwa **kukupa maelezo kuhusu lini itakuwa zamu yako ya chanjo.**

Chaguo3:

Je! unahitaji msaada? Piga simu ya chanjo **ya manispaa** namba **906 83 432**. Tunaelewa Kinorwei na Kiingereza. Tarajia muda fulani wa kusubiri pindi upigapo simu.

Ni nini hufanyika pindi ninapokuwa nimejiandikisha?

Mara baada ya kujiandikisha/kusajiliwa, utapokea ujumbe mfupi wa maandishi. Zamu yako ya kupata chanjo, utapokea ujumbe mpya **wa** maandishi ulio na **kiunga** cha mfumo wa miadi. Bonyeza kwenye kiunga **hiki ili uweke miadi haraka iwezekanavyo baada ya kupokea ujumbe** wa maandishi.

Haijulikani ni lini muda wa chanjo utafanyika, hii inategemea ni lini manispaa itapokea chanjo hizo. Ilani(kuitwa kupokea chanjo) **kunaweza kufanyika kwa** taarifa fupi.

Chanjo hiyo ina dozi **mbili ambazo lazima ziwekwe katika idadi fulani ya** wiki zilizoamuliwa. Mara baada ya kuweka miadi ya dozi ya kwanza ya chanjo, miadi mipya itaundwa kiotomatiki kwa ajili yako kwa dozi ya pili.

Chanjo hufanyika wapi?

Kimsingi, chanjo zote zitafanyika katika kituo cha chanjo, katika eneo(majengo) ya **zamani ya Bergan, Loe Bruk nr. 9 huko Loesmoen, Hokksund**. Katika hali maalum sana, wakazi binafsi wanaweza kupatiwa chanjo nyumbani.

Unataka taarifa zaidi?

[Bonyeza hapa kwa taarifa zaidi kuhusu chanjo dhidi ya Covid-19.](#)